

## Ninawi ni wapi?

Ninawi ni mji uliokuwepo kaskazini mwa **Taifa la Iraq** kwasasa. Mji huu kwasasa haupo, ila mahali pale ulipokuwepo mpaka leo pako!. Na mji huu ndio uliokuwa mji mkuu wa Taifa la Ashuru. (Kujua Taifa la Ashuru ni wapi kwasasa fungua hapa> **ASHURU**).

Mji wa Ninawi ndio Mji Nabii Yona aliagizwa na Mungu akahubiri Injili, ili watu wa mji ule watubu, lakini alikataa na kukimbilia mji wa Tarshishi. Kujua Mji wa Tarshishi kwasasa ni nchi gani basi fungua hapa> **TARSHISHI**.

Mji wa Ninawi haukuwa mji wenye watu wengi sana lakini ulikuwa umeendelea sana. Kipindi Nabii Yona anatumwa kwenda kuhubiri huko, biblia inarekodi mji ule kuwa na watu **120,000 tu!**.

*Yona 4:10 “Bwana akamwambia, Wewe umeuhurumia mtango, ambao hukuufanyia kazi, wala kuuotesha; uliomea katika usiku mmoja, na kuangamia katika usiku mmoja;*

*11 na mimi, je! Haikunipasa kuuhurumia Ninawi, mji ule mkubwa; ambao ndani yake wamo watu zaidi ya mia na ishirini elfu, wasioweza kupambanua katika mkono wao wa kulia na mkono wao wa kushoto; tena wamo wanyama wa kufugwa wengi sana?”*

Ijapokuwa Mungu alikusudia kuuadhibu mji huu lakini wenyeji wake walitubu kwa mahubiri ya Yona. Na Bwana Yesu alikuja kutoa unabii kwa vizazi hivi vyaa siku za mwisho kuwa..

*Mathayo 12:41 “Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa; KWA SABABU WAO WALITUBU KWA MAHUBIRI YA YONA; na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona”.*

Na sisi tunapaswa tutubu kwa mahubiri ya Bwana Yesu, ili tusije

kuangukia hukumu siku ya Mwisho.

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema,

Kwa maombezi/Ratiba za ibada/ Ushauri/ Maswali.

Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii

>> <https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

---

### **Mada Nyinginezo:**

*Babeli ni nchi gani kwasasa?*

***NINI MAANA YA KUTUBU***

*YONA: Mlango wa 4*

## Rudi nyumbani

Share on:

WhatsApp